# Deni Lina Waibia Wasichana Mustakabali Wao: Wito Wa Pamoja Wa Kuchukua Hatua

*“Wakati serikali zinalazimika kutumia zaidi kulipa madeni kuliko kugharamia wananchi wao, wasichana ndio wanaolipa gharama kubwa zaidi. Tunahitaji kurekebisha mifumo ya madeni iliyovunjika ili kuweka mahitaji ya wasichana balehe mbele ya masilahi ya wadai.” — **Malala Yousafzai***

**Mgogoro wa madeni unawaibia wasichana mustakabali wao — tunataka hatua zichukuliwe sasa**. Sisi ni wasichana, viongozi vijana wanawake, na watetezi wa haki za wasichana kutoka kote ulimwenguni, tunazitaka serikali, taasisi za fedha za kimataifa, wadai binafsi na nchi wadai — hususan zile za G20 — kukomesha madhara yanayosababishwa na madeni, na kuandika upya kanuni za mfumo wa madeni kwa ushirikiano na wasichana.

Zaidi ya asilimia 40 ya watu duniani wanaishi katika nchi zinazotumia fedha nyingi zaidi kulipa riba ya madeni kuliko kugharamia elimu au afya.Nchi kumi ambazo wasichana wanakabiliwa na vikwazo vikubwa zaidi katika kujifunza zinatumia fedha mara nne zaidi kulipa madeni kuliko kuwekeza katika elimu.Serikali zinapopunguza huduma muhimu ili kuwaridhisha wadai, wasichana balehe wananyimwa haki ya kupata elimu, huduma za afya na ulinzi wa kijamii — na hivyo kunaswa katika mzunguko wa udhaifu na kutengwa.

Sera za kubana matumizi zinazochochewa na madeni zinageuza haki ya kupata elimu ya bure, salama na bora kwa miaka 12 kuwa anasa ambayo wachache tu wanaweza kuimudu. Wasichana ndio wanaoathirika kwanza pale familia zinaposhindwa kumudu gharama za shule. Kodi kubwa kwa bidhaa za hedhi na kupunguzwa kwa programu za afya ya hedhi mashuleni kunawalazimisha wengi kubaki nyumbani wakati wa hedhi, na hivyo kuongeza hatari ya kuacha shule. Shule nyingi hazina rasilimali za kufundisha masomo muhimu kama elimu ya afya ya uzazi na haki za kijinsia, elimu ambayo ingeweza kuwawezesha wasichana na kupunguza ukosefu wa usawa wa kijinsia.

Kupunguzwa kwa huduma za afya na ustawi wa jamii kunawalazimisha wasichana balehe kujaza mapengo ya huduma za malezi, jambo linalowanyima muda wa kusoma na fursa za maendeleo. Wasichana wajawazito au wenye watoto wako hatarini zaidi wakati vituo vya afya vinapofungwa au kukosa wafanyakazi. Wasichana wanaokabiliwa na changamoto nyingi kwa pamoja — kama vile ulemavu,

> *“Elimu haipaswi kuonekana kama gharama ya kaya; kwa wasichana kama mimi, elimu ndiyo njia yetu kuu ya usalama na kujitegemea.”*
>
> — **Saira**, mwanafunzi wa sekondari, Pakistan

rangi au uhamisho — hulipa gharama kubwa zaidi kadri programu maalumu na jumuishi zinavyopunguzwa. Serikali zinapoendelea kuweka ulipaji wa madeni mbele hata wakati wa majanga ya hali ya hewa au migogoro, umasikini na ukosefu wa usalama huongezeka — na familia hulazimika kutumia mbinu hatarishi kama ndoa za utotoni au unyonyaji. Kupungua kwa uwekezaji katika elimu na ulinzi wa kijamii kunazidisha mzunguko wa kutengwa na umasikini kwa wasichana.

**Deni linawaweka wasichana hatarini — linawaibia ndoto zao na uwezo wao wa kuunda mustakabali wao.**

Serikali, taasisi na wadai binafsi wanaoamua sera za madeni si tu kwamba wanashindwa kuchukua hatua — bali wanadumisha mifumo inayowadhuru wasichana, huku wakikataa uongozi wao katika majukwaa muhimu ya kimataifa kama G20, Umoja wa Mataifa (ikiwemo COP), na hata katika majadiliano rasmi ya madeni.
Sisi ni muungano unaojitolea kutetea haki za wasichana, na tunasimama nao kama wenye haki na viongozi katika mapambano ya haki ya madeni.

Sisi ni muungano unaojitolea kutetea haki za wasichana, na tunasimama nao kama wenye haki na viongozi katika mapambano ya haki ya madeni.

> *“Rasilimali zikifika kwa wasichana wanaozihitaji zaidi, hatuondoi tu vizuizi kama gharama ya taulo, bali tunaunda mazingira ambamo kila msichana anaweza kubaki shuleni, kujifunza na kustawi.”*
>
> **— Sa’adatu Saidu Idris,** mwanaharakati wa elimu ya wasichana, Nigeria



## Pamoja, tunatoa wito wa mageuzi ya kimataifa katika mfumo wa madeni ambayo yatahakikisha kuwa dunia inawajibika kwa wasichana, si kwa wadai. Tutashinikiza mageuzi ya kimataifa ya madeni ambayo:

1. **Yanayokomesha madhara yanayosababishwa na madeni sasa hivi.** Wadai wote — wakiwemo IMF — wanapaswa kukomesha mara moja masharti yanayolazimisha serikali kupunguza huduma muhimu. Sera hizi za kubana matumizi zinawanyima wasichana haki zao, zinawaweka hatarini, na zinaiba mustakabali wao.

2. **Yanaziba pengo la ufadhili wa haki za wasichana**. Mageuzi ya mfumo usio wa haki wa madeni — sambamba na sheria za kimataifa za ufadhili zenye usawa zaidi — yanaweza kufungua mabilioni ya dola kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na haki za wasichana. Kuweka kikomo cha ulipaji madeni hadi asilimia 10 ya mapato ya taifa kunaweza kufungua dola bilioni 506 kwa elimu katika kipindi cha miaka mitano. Serikali lazima zihakikishe bajeti zinazozingatia usawa wa kijinsia ili fedha hizi ziweze kufika kwa wasichana na kubadilisha maisha yao.

3. **Zinahakikisha ushiriki wa maana wa wasichana na wanawake vijana katika maamuzi ya madeni.** Wasichana na wanawake vijana lazima watambuliwe kama wenye haki na wataalamu katika mchakato wa sera na maamuzi ya madeni. Serikali, taasisi za fedha za kimataifa na taasisi za wadai zinapaswa kutoa nafasi rasmi kwao kushiriki kikamilifu, kusikilizwa, na kushawishi maamuzi yanayowahusu.

4. **Zinajenga ulinzi madhubuti katika mifumo ya madeni ili kuzuia madhara zaidi au kutengwa**. Taasisi za fedha za kimataifa, wadai wote (wa serikali na binafsi) na mashirika ya utoaji wa viwango vya mikopo lazima wafanye mageuzi ya kimsingi katika mfumo wa madeni duniani. Mchakato, makubaliano na zana za tathmini za madeni lazima ziweze kutambua na kujibu ipasavyo mahitaji, vipaumbele na haki za wasichana katika muktadha wa madeni.

## Mabadiliko Tunayohitaji

- **Viongozi wa G20 lazima wakubaliane kufanya mageuzi ya G20 Common Framework on Debt Treatments** ili kutoa msamaha wa madeni wa kina, wa haraka na wenye muda maalumu — wakisitisha malipo yote ya madeni wakati wa majadiliano na kuweka kipaumbele kwa haki za wasichana.

- **Taasisi za fedha za kimataifa na wadai wote lazima waache mara moja** kulazimisha sera za kubana matumizi kwa serikali zenye kipato cha chini, wasitishe moja kwa moja ulipaji wa madeni wakati wa migogoro, waweke ukomo wa ulipaji wa madeni kwa 10% ya mapato ya taifa, na walinde matumizi ya kijamii. Wasaidie pia kuendeleza bajeti zinazozingatia usawa wa kijinsia, kwa mujibu wa Ajenda ya Addis Ababa na Compromiso de Sevilla. Ianzishwe Bodi ya Ushauri ya Vijana na Asasi za Kiraia ya kudumu. Madeni yote yasiyodumu au yasiyo halali yasamehewe.

- **IMF na Benki ya Dunia** lazima zirekebishe mbinu za tathmini ya uhimilivu wa madeni ili ziakisi uwezo wa nchi kutimiza malengo ya haki za binadamu, usawa wa kijinsia na tabianchi. Vitengo vya jinsia ndani ya taasisi hizi vipate ufadhili na mamlaka kamili. IMF irekebishe sera yake ya "social spending floors" ili iendane na viwango vya kimataifa vya ulinzi wa kijamii vinavyolinda haki za wasichana — na iweke viwango hivyo kuwa ahadi za wazi na zenye matokeo halisi, badala ya kubana matumizi.

- **Serikali lazima zikubaliane kuhusu Mkataba Mpya wa Umoja wa Mataifa kuhusu madeni ya kitaifa (U.N. Framework Convention on Sovereign Debt)**, unaolinda haki za binadamu, uwazi na uwajibikaji — huku wasichana na wanawake vijana wakiwa sehemu muhimu ya muundo, utekelezaji na ufuatiliaji kupitia ushiriki wa kiraia na nchi wanachama.

- **Serikali za kitaifa,** ikiwemo zile zilizo na madeni makubwa, lazima zitekeleze ahadi zao kwa wasichana chini ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Tamko la Beijing na Jukwaa la Utekelezaji, na mfumo wa kimataifa wa haki za binadamu. Zihakikishe:
  - Kipaumbele kwa matumizi ya umma, uchumi wa malezi, na bajeti zenye usawa wa kijinsia ili rasilimali kutoka msamaha wa madeni ziweze kufikia moja kwa moja utekelezaji wa haki za wasichana.
  - Ushiriki wa kiraia uwe wa kudumu na uwakilishi wa maana wa wasichana na wanawake vijana uhakikishwe.

- **Wabunge katika vituo vikuu vya kifedha** duniani lazima wapitishe sheria zinazowalazimisha wadai binafsi kushiriki katika msamaha wa madeni kwa masharti sawa, na kupiga marufuku mashauri ya kinyonyaji (predatory litigation) yanayolenga kupata faida zisizo za haki.

- **Benki za Maendeleo za Kimataifa** na nchi wadai lazima waongeze ufadhili wa ruzuku kwa miradi inayoongozwa na wasichana na yenye kulenga wasichana — zikitumia ufadhili rahisi, wa muda mrefu, unaofadhili gharama za msingi na kujenga uongozi wa wasichana.

- **Mashirika ya utoaji** wa viwango vya mikopo lazima yarekebishe mbinu zao ili kuzingatia uwekezaji katika maendeleo endelevu — ikiwemo haki za wasichana — na kuonyesha kwa uwazi manufaa ya kijamii na kiuchumi ya mageuzi ya madeni. Kwa muda mrefu, serikali zinapaswa kuanzisha taasisi ya umma ya kimataifa ya utoaji wa viwango vya mikopo inayohakikisha tathmini zenye haki, uwazi na zinazozingatia usawa wa kijinsia.

## Haki ya madeni ni haki ya wasichana. Jiunge nasi katika kuandika upya kanuni za mfumo wa madeni duniani, tukiwa na wasichana.

*Tamko hili limeandikwa kwa ushirikiano na wasichana na wanawake vijana kumi na mmoja mashuhuri kutoka sehemu mbalimbali duniani, likiwa na maoni kutoka kwa washirika zaidi ya ishirini, wakiwemo viongozi vijana. Kwa maelezo zaidi kuhusu tamko hili, tafadhali au wasiliana kupitia:* ***carron@malalafund.org***